**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA**

***Unapojibu tafadhali taja:***

**Kumb. Na. HB/W:20/02/455** **15/04/2025**

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA DEREVA KWA MKATABA WA MUDA MAALUM – NAFASI 3.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda anawatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi ya kazi ya Dereva kama ifuatavyo:-

## 1. SIFA ZA MWOMBAJI

a) Kuajiriwa mwenye cheti cha mtihani wa Kidato cha nne (IV), mwenye leseni daraja **"E"** au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
b) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
c) Wombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

## 2. KAZI NA MAJUKUMU:

a) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
b) Kuwapeleka Watumishi maeneno mbalimbali kwenye safari za Kikazi.
c) Kuhakikisha gari na vyombo vyake viko katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
d) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali za Serikali.
e) Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari
f) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika Daftari la Safari (Logbook).

## A. MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania
2. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye Anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees Watatu wa Kuaminika).
4. Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) Ziandikwe jina la mwombaji nyuma.
5. Testmonials Provisional results "Statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA**.
6. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za Kisheria.
7. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **29/04/2025** kabla au ifikapo **Saa 9:30 Alasiri.**

**MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa Pamoja na vyeti vya elimu, Anuani ya Barua ielekezwe kwa;

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Bunda,**
**S.L.P 126,**
**BUNDA.**

- Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta au Masijala ya Wazi ya Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.
- Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili, **HAYATAFANYIWA KAZI.**

Oscar J. Nchemwa,
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W),
**BUNDA.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA